

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO



TANGAZO LA KOTESHENI

Namba ya Kotesheni: LGA/079/2017-2018/HQ/NC/17 LOT 01

YA

UPANGISHAJI WA KITEGA UCHUMI CHA ROCK GARDEN

Tarehe 23/01/2018

1. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inatangaza kupangisha kitega Uchumi cha Rock Garden kilichopo katika makutano ya barabara ya Rwegasore na Boma. Bustani hiyo ina ukubwa wa ekari nne (4) na iko umbali wa kilometa tatu (3) kutoka katikati ya mji. Biashara inayofanyika katika bustani hiyo kwa sasa ni uuzaji wa vinywaji vikali na baridi. Bustani hiyo inafaa kutumika kama kivutio cha utalii chenye Mazingira ya uoto wa asili, sehemu za mapumziko katika siku za mwisho wa wiki na shughuli mbalimbali za burudani.
2. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inakaribisha maombi ya zabuni toka kwa Makampuni, Mashirika, Vikundi vya watu binafsi wenye sifa za kufanya ukarabati kuboresha bustani hiyo na kuendesha Biashara kwenye eneo hilo kwa kipindi cha miaka mitatu (3).
3. Mkataba wa upangishaji ni wa miaka mitatu (3) na utafanyiwa mapitio "review" ya kiwango cha kodi baada ya miezi kumi na minane (18).
4. **Sifa za muombaji:**
 - I. Awe na uwezo wa kifedha wa kutosha kwa ajili ya kufanya ukarabati mdogo kama ilivyoonyeshwa kwenye maelezo ya kazi (Bill of Quantities) iliyoambatanishwa kwenye kitabu cha zabuni. Gharama za ukarabati huo zitarejeshwa kupitia asilimia sitini (60%) ya kodi ya pango itakayobaki kwa mpangaji baada ya kulipa asilimia arobaini (40%) ya kodi ya pango kwa mwenye mali.
 - II. Awe na uwezo wa kifedha kwa ajili ya kuendesha Biashara atakayoifanya kwenye eneo hilo pamoja na kuboresha Mazingira ya bustani hiyo.

- III. Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) katika uendeshaji wa Biashara anayopanga kuifanya katika eneo hilo.
 - IV. Awe na namba ya mlipa kodi (TIN Number).
 - V. Awe na uwezo wa kulipa asilimia arobaini (40%) ya kodi ya pango iliyokubaliwa na mwenye mali kwa kila mwezi kwa kiwango kitakachokubaliwa na Manispaa kwenye zabuni. Kodi ya pango italipwa siku (5) kabla (in advance) ya mwezi ya upangishaji kuanza.
 - VI. Asiwe mdaiwa wa Manispaa ya Morogoro wala taasisi nyingine ya Umma.
5. Watoa huduma wenye nia ya kupanga kwenye bustani hiyo wanaweza kukagua nyaraka za zabuni na kupata maelezo kutoka kwa Katibu wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro S.L.P. 166 siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu za kitaifa .
 6. Nyaraka ya zabuni inapatikana kwa kuleta barua ya maombi na malipo ya Fedha taslimu yasiyorudishwa (Non refundable) ya shilling **Elfu Hamsini tu (50,000/=)** kwa Mkurugenzi wa Manispaa S.L.P. 166 Morogoro.
 7. Zabuni zote ikiwa ni nakala halisi moja (1) pamoja nakala vivuli mbili (2) zilizojazwa kwa ufasaha na kufungwa kwa lakiri kwenye bahasha isiyokuwa na alama yoyote zitumwe kwa:- Katibu Bodi ya zabuni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro S.L.P. 166 Morogoro.
 8. Zabuni zote ziwasilishwe kwenye sanduku la zabuni, lililopo kwenye ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Morogoro Au zitumwe kwa kifurushi Maalum (Registered Mail) ili zifike kabla ya tarehe na muda wa mwisho wa uwasilishaji zabuni uliioonyeshwa kwenye aya ya 9 hapo chini.
 9. Mwisho wa kupokea zabuni ni Ijumaa Tarehe 29/01/2018 saa 6:00 Mchana na mara baada ya hapo Zabuni zitafunguliwa kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa. Wazabuni wote wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi huo. Bahasha ya nje iandikwe **KOTESHENI NA. LGA/079/2017-2018/HQ/NC/17 LOT 01 YA UPANGISHAJI WA KITEGA UCHUMI CHA ROCK GARDEN . ISIFUNGULIWE KABLA YA SAA SITA 6:00 MCHANA TAREHE 29/01/2018**
 10. Zabuni ambazo hazitapokelewa, kufunguliwa wala kusomwa wakati wa ufunguzi hazitashugulikiwa .

John K. Mgalula
**MKURUGENZI WA MANISPAA,
MOROGORO.**